

Insha ya Ratiba - Kiswahili Insha Notes

- Ratiba ni orodha ya mpangilio wa namna mambo yatakavyofuatana katika shughuli fulani.
- Lengo lake ni kuhakikisha wakati unatumiwa vizuri ili mambo fulani yasije yakakosa kutendwa kutokana na upungufu wa wakati.
- Ratiba hutumika katika sherehe, mikutano, mazishi, hafla, tamasha, n.k

Sehemu za Ratiba

1. Kichwa

- Kichwa cha ratiba hutaja mambo yafuatayo:
 - Shughuli yenyewe - Taja jina la tukio ambalo unaandalia ratiba. Kwa mfano Harusi ya Bwana na Bi Arusi, Siku ya Zawadi
 - Tarehe ya shughuli - je shughuli hiyo itafanyika lini?
 - Mahali- Taja mahali ambapo shughuli hiyo itafanyikia. kwa mfano katika uwanja wa michezo wa Kasarani, kanisa la St. Mtakatifu
- Mfano wa kichwa cha ratiba:
 - Ratiba ya Hafla ya Ukimwi katika Bustani la Uhuru tarehe tano Januari.
 - Ratiba ya Mazishi ya Dkt. Marehemu tarehe 20/12/1923 Kijijini Vikwazoni

2. Mwili

- Mwili wa ratiba hujumuisha mambo mbalimbali yatakayofanyika katika mpangilio maalum, saa mbalimbali. Ni vizuri kuzingatia vipengele vifuatavyo:
 - Saa - Onyesha saa ambazo tukio limepangiwa kuanza hadi linapotakiwa kumalizika
 - Mahali - Ikiwa shughuli tofauti zinafanyika katika mahali mbalimbali kama vile vyumba tofauti, inapaswa hutaje mahali ambapo kila jambo litafanyikia.
 - Wahusika - Taja mtu au watu waliopewa wajibu wa kutekeleza jambo fulani. Hii huwasaidia kujitayarisha ipasavyo.

Mfano wa Ratiba

RATIBA YA MAZISHI YA MZEE MAUTI TAREHE 20/12/1923 KIJIJINI MIZUKANI

SAA	SHUGHULI
07: 00	Marafiki wa Mauti watoa mwili kutoka SlowDeath Hospital
10: 30	Maombi katika kanisa la G.I.Z.A yakiongozwa na Pst. Muna Fiki
11: 15	Mwili kuwasilishwa nyumbani, familia ya Mauti
12: 00	Kupakuliwa kwa chakula na Bi Kamafisi, Bi Mwachafu na wapishi walioteuliwa
1: 10	Kukusanyika kwa umati
2: 00	Maombi ya kuanzisha shughuli za mazishi
2: 30	Shuhuda zikiongozwa na Mzee Siachwinyuma
3: 00	Ushuhuda wa serikali na Chifu Mtesi
3: 40	Kuteremshwa kwa mwili kaburini na vijana walioteuliwa
4: 00	Shukrani za Mwisho, na Mwenyekiti wa Chama cha Kufa Tukusaidie
6: 00	Kugawana mali ya marehemu, na wazee wa kijiji